

LUGHA YA KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

Saa 2 Dakika 30

STANDARD HIGH SCHOOL ZZANA

Uganda Certificate of Education

LUGHA YA KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza

Muda: Saa Mbili na Nusu

MAAGIZO KWA WATAHINIWA:

Jibu Maswali manne kwa jumla. Mawili kutoka kila sehemu.

Swali la kwanza lina sehemu mbili yaani A na B.

Chagua sehemu mojawapo ama A au B.

SEHEMU A

Ama

1. (a) Andika insha isiyopungua maneno 400 wala kuzidi 450 juu ya mojawapo ya mada zifuatazo; (Alama 40)
- (i) Umuhimu wa Elimu Nchini
 - (ii) Siku kuu iliyokufurahisha sana
 - (iii) Mshika mbili moja humponyoka
 - (iv)kwa kweli Wahenga hawakukosa waliponena kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika mguu.

Au

- (b) Andika insha **mbili** fupi zisizopungua maneno 150 wala kuzidi 250 juu ya miktadha miwili ifuatayo.
- (i) Andika hotuba utakayopenda kutoa wakati wa kusherekea siku ya kuzaliwa kwako.
 - (ii) Andika mazungumzo kati ya polisi na mwizi.
 - (iii) Kaka yako aliondoka nyumbani mwaka jana na kwenda kufanya kazi katika nchi jirani. Tangu aondoke, hamjapata kuonana wala kuwasiliana naye. Mwandikie barua ukimjulisha hali za nyumbani na za kisisasa nchini mwako.
 - (v) Wewe ni katibu wa chama cha Kiswahili shulenii mwako. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika kuhusu maendeleo ya Chama.

UFAHAMU

2. **Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.** (Alama 20)

Kiswahili ni Luga ya Kiafrika iliyotokea kutokana na mwingiliano wa maneno hususa ya Kibantu na Kiarabu. Kiswahili ni Kibantu na siyo Kiarabu kama watu wengine wasemavyo. Asili ya Kiswahili inaaminika kuwa pwani ya Afrika Mashariki. Hapa ndipo waarabu kutoka Uarabuni waliposhirikiana na waafrika katika shughuli mbalimbali .Na katika shughuli zao walikuwa wanachanganya maneno ya kibantu na kiarabu ili waweze kuwasiliana na kuelewana vizuri. Matokeo yake yakaunda lugha ya mseto. Lugha hiyo mpya ikaja kuwa Kiswahili.

Kuna sababu nyingi zilizosaidia Kiswahili kuenea na kusambaa kwa mwendo wa kasi duniani; Biashara, Dini, Ndoa kati ya waarabu na waafrika, Ukoloni, Afrika kupata Uhuru , vyombo vya habari, Elimu, siasa za kizalendo, uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili, ukuaji wa teknolojia,Uhamaji na uhamiaji, utendawazi.

Kiswahili ni lugha ya kibantu na hii ni kwa sababu asilimia kubwa kwa takriban asilimia sabini na tano ya maneno yanayotumika katika Kiswahili yanapatikana kwenye lugha nyingi za kibantu.

Miaka ya karne ya kumi, mataifa ya mbali yalijaribu kuja Afrika ya Mashariki, hasa mataifa ya mashariki ya mbali kama Waarabu, Waajemi, Wahindi na hata Wachina. Kilichowaleta kilikuwa zaidi ni biashara. Kwa sababu labda ya umbali, mataifayao hayo hayakuja kwa wingi kama Waarabu. Waarabu waliishi karibu na Afrika na walizidi kupenda Afrika Mashariki kwa ajili ya biashara ya Watumwa, pembe za ndovu na isitoshe dini ya Kiislamu ilipoanzishwa huko Uarabuni, walitaka kuieneza mbali. Waarabu wengine walikuja pande hizi ili kuieneza dini hiyo na walipata wafuasi wengi.

Katika hizo *hekaheka*, mwingiliano zaidi ultiokena kwani Waarabu wengine walioa wanawake wa Kiafrika. Isitoshe, Waarabu hakuwa namakuukama mataifa mengine kwa hivyo walipatana na wenyeji zaidi ya vile wenyeji walivyochukuana na mataifa mengine. Katika hizi pilikapilika, Kiswahili ambacho kilikuwa kinaingiliana na lugha nyingine za Kibantu kwa kasi kiliathiriwa pia na lugha nyingine za kigeni hasa Kiarabu. Ndio maana leo Kiswahili kina zaidi ya asilimia thelathini na tatu ya msamiati wa asili ya Kiarabu, kiasi ambacho ndicho kikubwa sana cha mkopo wa maneno hasa ukilinganisha na maneno ya mataifa mengine.

Wavumbuzi kama Livingstone, Speke, Grant, Burton, kina Baker na Henry Murton Starnley, walipofika sehemu hizi za Afrika, watu wa Ulayawalizidi kuvutiwa na Bara la Afrika hasa Afrika Mashariki. Wavumbuzi hawa walijua kuwa kulikuwa na shughuli za biashara ya watumwa na hazikuwapendeza watu hawa wa Ulaya. Wareno nao hawakupendezwa kuwaona Waarabu ambao tayari walikuwa wamejikita sawa sawa na kuzitawala baadhi ya sehemu za huku Afrika Mashariki. Waliwalinganisha na Waarabu majirani zao, wa Afrika ya Kaskaziniwaliorwita *Moores*. Hao Moores walikuwa wameshapigana vita na Wareno walishindwa. Chuki hiyo iliendelezwa walipowaona Waarabu wa Afrika Mashariki. Jambo hili liliwafanya wasiwe na mazoea sana na wenyeji wa Afrika ya Mashariki. Athari za lugha basi zilizoachwa na Wareno ni kidogo sana. Ni kama, ‘meza na mvinyo’.

Mashirika ya dini huko Ulaya yalitaka Waafrika wafunzwe dini na kukomesha biashara ya watumwa. Walitaka kujua zaidi juu ya Afrika Mashariki. Wamisheni na wavumbuzi Krapf na Rebmann, walitumwa na shirika la dini lililoitwa ‘The Church Missionary Society’ huko Rabai Pwani. Wajerumani nao waliendesha mambo ya dini ya kuanza kukomesha biashara ya watumwa. Maenezi ya dini

yaliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Askofu Edward Steere alianzisha maandishi kwa Kiswahili. Jinsi shughuli za kidini zilivyoendelea kutumia Kiswahili na jinsi maandishi kwa lugha ya Kiswahili yalivyozidi, ndivyo Kiswahili kilivyoendelea kusambaa na kuenea vururu duniani. Kamusi ya kwanza ya Kiswahili iliandikwa na Daktari Ludwig Krapf.

Waarabu nao kufikia miaka ya karne ya kumi na tisa, walikuwa wamepenya mbali, wengi wakiwa wamefika hadi Kongo na Uganda. Wengine walishika hatamu uongozini, hasa sehemu za Zanzibar. Kiswahili kilizidi kutumika hasa katika miji na zile sehemu zilizokuwa njia kuu za kusafirishia watumwa.

Huko Ulaya nako wakati huo kulikuwa na mashindano ya kibiashara. Walitaka mahali pa kutawala ili wawe na mahali pa kupatia malighafi na nguvu za kiuchumi. Kufikia mwaka wa 1873 bwana John Kirk, Muingereza aliyekuwa ni mshauri wa Uingereza aliandika mkataba na Seyyid Barghash kuhusu Waarabu kuacha biashara ya watumwa na Waarabu kutawala maili kumi za mwambao wote wa pwani. Waingereza hawakuonekana mwanzoni kuwa na haja ya kutawala sana ingawa baadaye walitawala Kenya na Uganda. Baadaye Mjerumani kwa jina Karl Peters aliandikisha mikataba na wakuu wa kienyeji na huo ukawa mwanzo wa utawala wa Kijerumani huko Tanganyika.

Watawala hawa walijaribu kukitumia Kiswahili na kukiruhusu kitumike katika shughuli za utawala, dini na kazi mashambani. Maandishi yalizidi kuandikwa kupitia magazetini, vitabuni na shule zilianzishwa na wanafunzi walifunzwa Kiswahili. Miji ilikua na watu walizidi kukutana na kutumia Kiswahili. Lakini mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda. Kama hawa watawala wangekikataza Kiswahili pengine kisingepiga hatua kubwa.

Mgala muue na haki umpe. Ingawa wazungu wengine walikuwa wakatili, kulikuwa nawengine waliokipenda na kukiendeleza hata kimaandishi. Ilipofikia mwaka wa 1925, Gavana wa Tanganyika, Muingereza, aliona haja ya kuisanifisha lugha. Aliitisha mukutano wa Afrika Mashariki na kutaka kuanzishwe baraza la Kiswahili la kusanifisha lugha.

Kiswahili kilisanifisha sana kuunganisha watu na kilitumika sana shulenii, mijini, redioni, magazetini, kwenye sahani za santuri, katika michezo ya kuigiza, vitabuni, televisheni na hata sasa kinazidi kutia fora kwani kimefanywa somo la lazima na kinazungumzwa na mamilioni ya watu duniani hasa Afrika Mashariki.

MASWALI:

- (a) Pendekeza mada mwafaka kwa taarifa ya habari hiyo. (Alama 02)
- (b) Nini maana ya Kiswahili? (Alama 01)

- (c) Kwa nini Waarabu walikopesha lugha ya Kiswahili maneno mengi kuliko mataifa mengine? (Alama 01)
- (d) Kwa nini mwandishi amesema, ‘Mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda’? (Alama 02)
- (e) Ni mataifa gani ambayo yaliingiliana na Waafrika wa Afrika Mashariki kabla ya karne ya ishirini? (Alama 02)
- (f) Wavumbuzi na wamisheni walisa diaje katika ukuaji wa Kiswahili? (Alama 03)
- (g) Ni sababu gani zilizofanya mataifa mengine yapende kuja Afrika Mashariki? (Alama 02)
- (h) Ni sababu gani zilizoimarisha maenezi ya Kiswahili? Fafanua sababu nne. (Alama 04)
- (i) Andika methali yoyote moja iliyotumiwa katika habari hiyo. (Alama 01)
- (j) Hawa ni watu gani katika habari hiyo? (Alama 02)
 - (i) Wamisheni
 - (ii) Wavumbuzi
 - (iii) Wakoloni

SEHEMU B

3. Soma habari ifuatayo kisha uifupishe kwa maneno 90; (Alama 20)

Serikali za nchi nyingi zinatilia maanani suala la elimu. Kila nchi huakikisha kwamba kila mwananchi au raia hupata elimu iliyo bora na mwafaka katika ujenzi wa taifa kwa kuchochea maendeleo katika nyanja mbalimbali. Hata hivyo, inasikitisha kuwa idadi kubwa ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika, hususa katika nchi zinazoendelea. mtu ambaye hajui kusoma wala kuandika anaitwa mjinga kwa lugha ya kiswahili. Kuna matatizo au kasoro za kukosa elimu nyingi kwa mfano; kutoweza kusoma na kuandika, kudanganywa katika hesabu na kupata hasara ya pesa, siri za mjinga zote zitaweza kufichuka kwa sababu hawezi kujisomea maandishi mwenyewe hata ikiwa barua ya siri. Mjinga vilevile anaaibika kwa kukosa kujielezea mbele ya watu, atashindwa kujiamini.

Idadi ya wajinga itaendelea kuongezeka maradufu mwaka baada ya mwaka ikiwa taifa letu halitatilia mkazo suala la elimu bora ili wananchi wake waweze kujiepusha na janga hilo.

Ujinga au ujahili ni ile hali ya mtu kutojua kusoma wala kuandika. Je, kujua kusoma na kuandika ni jambo muhimu au la? ukweli ni kwamba elimu ni jambo muhimu sana kulingana na sababu zifuatazo; kwanza kabisa, mtu anayejua kusoma na kuandika

atakuwa na uwezo wa kupanga matumizi mazuri ya pesa ya kila siku bila ya kuenda hasara. Isitoshe, atakuwa na uwezo wa kuwekeza na kupanga mapato yake ndani ya muda fulani. Ataweza pia kuwasiliana na wateja wake bila ya kutegemea watu wengine. Halikadhalika, mtu ajuaye kusoma na kuandika ataweza kupanga maisha yake ya mustakabali vizuri na kwa hivyo, atapata ufanisi na kuchochea maendeleo nchini mwake.

Kwa upande mwingine, kuna wananchi ambao wanajua kusoma na kuandika lakini hawatumii silaha ya uwezo wao. Hawawezi kupanga mapato na matumizi yao, na wanaendeleo kulalamika na kunung'unika kwamba uchumi wao ni duni, mapato yao ni duni, maisha ni magumu na umaskini ni mwingi. kinanachoshangaza kwa watu kama hawa ni kwamba wanayo elimu kubwa, lakini wanapopata fedha wanazifua kwa siku tu. punde si punde, wanabaki kuteseka kwa mwezi mzima.

Mtu aliyekosa kusoma utotoni, kwa sasa anayo bahati na nafasi ya kujiendeza kimasomo. Anaweza kujifunza kusoma na kuandika katika shule za watu wazima zinazoitwa '*ngumbaru*'. vilevile, *ngumbaru* ni elimu ya watu wazima. Serikali yetu inawahimiza watu wazima wajifunze kusoma na kuandika. kwa bahati mbaya, watu wazima ambao hujitokeza na kuijunga na shule za *ngumbaru* ni wachache mno. watu hawa wazima wanajiona kama wazee na hawaoni faida yoyote ya kujisumbua na haya masomo ya ukubwani. Wengine wanafikiri kuwa akili zao nazo zimezeeka, kustaafu na zimeshupaa na hivyo, haziwezi kushika masomo kwa urahisi. Baadhi yao wanasema kwamba hata wakijielimisha, umri wao mkubwa hautawawezesha kupata kazi. Mionganoni mwa mambo mengine yanayowasumbua watu wazima na kuwakosesha kuijunga na *ngumbaru* ni tabia zao mbaya. kwa mfano; ulevi wa pombe na uvutaji wa sigara na bangi, kuchanganya wanawake na wanaume kunasababisha uzinifu, kukata tamaa maishani, uvivu na kutotaka kufanya kazi.

4. Tafsiri habari ifuatayo kwa Kiswahili

(Alama 20)

At first, Ikemefuna had been frightened. But he was not frightened anymore because Okonkwo was walking right behind him. Ikemefuna felt safe. Okonkwo was like a real father to him. Ikemefuna had never liked his own father and he had forgotten him after three years but he loved Okonkwo.

Suddenly one of the men walking behind Ikemefuna made a noise in his throat. Ikemefuna looked around and the man told him to walk on and not to look back. He spoke in a frightening voice. His voice made Ikemefuna's whole body go very cold. Ikemefuna became frightened, his hands shook a little as they held the pot of wine. Ikemefuna looked back again quickly. Okonkwo was not walking behind him now. He was right at the back of the line of men.

Ikemefuna's legs began to shake. He was afraid to look back again. The man behind him raised his machete quietly and quickly and brought it down on Ikemefuna's head. Okonkwo heard the machete hit the pot of wine. The pot fell off Ikemefuna's head and broke on the ground. Okonkwo heard Ikemefuna cry out.

“My father, they have killed me, “Ikemefuna cried. Ikemefuna ran towards Okonkwo. Okonkwo was very afraid but he raised his own machete and brought it down on Ikemefuna’s head and killed him. Okonkwo did not want to do this. He was very afraid and he loved Ikemefuna but he was afraid that his friends would think he was weak if he did not kill Ikemefuna.

MATUMIZI YA LUGHA-SARUFI

5. Jibu kulingana na maagizo ya kila swali;—
 - (a) Kanusha sentensi zifuatazo;
 - (i) Nikikupenda, utanipenda pia? (Alama 01)
 - (ii) Ulikuwa umefanya kazi usiku kucha. (Alama 01)
 - (b) Tumia nahau hizi katika sentensi;
 - (i) Kula chumvi nyingi (Alama 01)
 - (ii) Kuaga dunia (Alama 01)
 - (c) Andika vinyume vya sentensi zifuatazo;
 - (i) Kifungua mimba wangu ni mtoto wa kiume. (Alama 01)
 - (ii) Maskini alimuuliza tajiri maswali machungu. (Alama 01)
 - (d) Hawa ni watu gani?
 - (i) Nahodha. (Alama 01)
 - (ii) Seremala. (Alama 01)
 - (e) Weka sentensi zifuatazo kwenye Usemi wa taarifa;
 - (i) “Ala! Kumbe John wewe ndiye mwizi! Nitakufunga!”, Hakimu alishangaa. (Alama 02)
 - (ii) “Nitawapigeni nyinyi nyote”, Mwalimu Kisitu aliwaonya wanafunzi.
 - (f) Tumia kiulizi –pi? Katika sentensi zifuatazo;
 - (i) Ni maji yaliyochemshwa? (Alama 01)
 - (ii) Barua iliwekwa mahali? (Alama 01)

- (g) Kamilisha methali zifuatazo;
- (i) Mtoto umleavyo..... (Alama 01)
- (ii)ila mzaliwa nawe. (Alama 01)
- (h) Ziweke sentensi zifuatazo kwenye Umoja;
- (i) Miwa iyo hiyo ndiyo itakayouzwa. (Alama 01)
- (ii) Nyimbo zizo hizo ndizo zitakazozinduliwa. (Alama 01)
- (i) Ziweke sentensizifuatazo Katika hali ya Kutendwa;
- (i) Mkunga alikuwa anamzalisha mama mjamzito. (Alama 01)
- (ii) Manchinga mzee anauza bidhaa mtaani. (Alama 01)
- (j) Andika tarakimu kwa maneno;
- (i) 15:45 Hours (Alama 01)
- (ii) 9,666,999 (Alama ½)
- (iii) 0.038% (Alama ½)